*Mulika, Juz. 44(2), 313-323*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Uchunguzi wa Mandhari katika Ujenzi wa Usaliti: Mifano kutoka Diwani ya *Wasakatonge* ya M. S. Khatib

*Baraka Sikuomba*[1] *na Shani Omari Mchepange*[2]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t2.9

**Ikisiri**

Makala hii inashughulikia mandhari katika ujenzi wa usaliti katika diwani ya *Wasakatonge* ya Muhammed Seif Khatib ambayo ilisomwa na watafiti na mandhari zote zilizosawiri usaliti[3] kudondolewa kwa kuzingatia lengo la makala, yaani kuchambua jinsi mandhari zinavyojenga usaliti katika diwani teule. Mandhari zilizotumiwa na mwandishi kujenga usaliti katika diwani teule ni pamoja na Afrika, ufukweni, sehemu za ibada, ikuluni na hospitalini. Uwasilishaji na uchambuzi wa data uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Mbinu kuu ya ukusanyaji wa data ilikuwa usomaji makini na uchanganuzi wa data ulifanyika kwa kutumia mbinu ya kitaamuli. Matokeo yanaonesha kuwa mandhari zinapotumiwa kwa ustadi mkubwa huunda usaliti kama tendo linalofichwa ndani ya hisani, tendo linalokumbatiwa katika kivuli cha uongozi, tendo linalotumika kutekeleza mauaji, tendo lililofichwa ndani ya mwamvuli wa dini, na tendo linalotumika kuendeleza matabaka. Makala hii imeongeza maarifa katika fasihi kupitia ushairi wa Kiswahili kwa kupanua uga wa uelewa wa kipengele cha mandhari katika kazi za ushairi kama ilivyo katika tanzu nyingine za riwaya, tamthiliya na hadithi fupi.

## 1.0 Utangulizi

Makala hii inahusu mandhari na ujenzi wa usaliti katika ushairi andishi wa Kiswahili kupitia diwani za *Wasakatonge* (2003) ya mwandishi Muhammed Seif Khatib. Uteuzi wa diwani hii umetokana na sababu kwamba ina kiwango kikubwa cha mandhari zinazoakisi usaliti wa wahusika. Rachmani (2010) anaeleza kuwa usaliti ni hali ya kupoteza imani na matarajio anayokuwa nayo mtu kwa mtu baada ya taasisi kuvunjwa. Si hivyo tu, bali matokeo ya usaliti katika jamii yameelekea kuacha uharibifu mkubwa katika maisha ya mtu binafsi na hata taasisi kiasi cha kuharibu uhusiano wa mtu na mtu au mtu na jamii (Oing, 2017). Miongoni mwa masuala hayo ya kijamii ni suala la usaliti ambalo halijawekwa bayana na watafiti waliochunguza diwani teule. Licha ya kuwa usaliti unapoteza uaminifu baina ya

[1] Mhadhiri, Idara ya Lugha, Chuo Kikuu Kishiriki cha Marian (Bagamoyo), Baruapepe: 1987baraka@gmail.com

[2] Profesa Mshiriki, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Baruapepe: shaniom@yahoo.co.uk

[3] Usaliti ni hali inayotokea katika mandhari yoyote ya uhusiano ambapo upande mmoja au mwingine unakiuka matarajio muhimu ya uhusiano baina ya marafiki (Wiseman na Duck, 1995).

ndugu au marafiki kiasi cha kusababisha migogoro katika mandhari mbalimbali, bado tafiti nyingi hazijamakinikia kipengele hiki kwa kina kupitia mandhari zinazojitokeza katika ushairi wa Kiswahili. Kutokana na umuhimu wa mandhari katika kazi za kifasihi, hususani ushairi wa Kiswahili, makala hii imechunguza namna mandhari zinavyoujenga usaliti katika diwani teule. Kimpangilio, mbali na utangulizi, makala hii imejumuisha kipengele cha muhtasari wa diwani teule, methodolojia, nadharia ya utafiti, matokeo ya utafiti na mjadala na hitimisho la jumla. Vipengele hivi vinajitokeza kama ifuatavyo:

## 2.0 Muhtasari wa Diwani Teule

Kabla ya kuchambua usaliti ulivyojengwa na mandhari katika diwani teule, sehemu hii inawasilisha muhtasari kuhusu diwani teule. Diwani ya *Wasakatonge* ni kazi iliyoandikwa na Muhammed Seif Khatib na kuchapishwa kwa mara ya kwanza na kampuni ya Oxford University Press mwaka 2003.. Diwani hii imesheheni mashairi yanayozungumzia hali ya wanajamii wanaofanya kazi duni na za sulubu ili kujipatia riziki ya kila siku. Katika diwani hii, mtunzi anaonesha hali ngumu ya maisha iliyopo katika jamii. Vilevile, Khatib anaonesha namna watu wanavyopambana kufanya shughuli mbalimbali kama vile za ubebaji mizigo bandarini kwa minajili ya kujikwamua kiuchumi. Pia, diwani hii inaonesha athari za matabaka katika jamii.

## 3.0 Methodolojia

Data iliyotumika katika makala hii imekusanywa kwa njia ya usomaji makini katika diwani ya *Wasakatonge* (2003). Baada ya kusoma diwani hii, jumla ya mashairi saba yaliyokidhi lengo la makala yaliteuliwa, hususani yaliyosheheni mandhari zinazosawiri suala la usaliti. Mashairi yaliyochaguliwa ni “Tiba Isotibu”, “Madikteta”, “Sikuliwa Sikuzama”, “Uasi”, “Wasakatonge”, “Mumiani” na “Wafadhiliwa”. Mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumika kupata mashairi saba kutoka katika diwani hii. Data katika mashairi hayo zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji makini. Mashairi teule yalisomwa na watafiti kwa kutumia mbinu ya usomaji makini, kisha data zilidondolewa kulingana na lengo la makala hii. Mwisho, uchambuzi na uwasilishaji wa data umefanywa kwa kutumia mkabala wa kimaelezo kwa sababu unafafanua kwa kina data ili kuzifanya zieleweke.

## 4.0 Kiunzi cha Kinadharia

Uchambuzi wa data katika makala hii uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Nadharia ya Uhalisia inarejelea mtindo wa uandishi unaojishughulisha na uwasilishaji wa picha halisi ya maisha ya watu katika jamii. Nadharia hii ilianzishwa mahususi kwa lengo la kuupinga mkabala wa ulimbwende uliokuwa umeshika mizizi mpaka kufikia karne ya 19 (Dargan, 1932). Katika mawanda ya fasihi, uhalisia wa matatizo yaliyokuwa yakiwakabili watu uliwafanya wanasanaa kuikosoa Nadharia ya Ulimbwende ambayo ilijikita katika matamanio ya kinjozi zaidi ikilinganishwa na taabu zilizokuwa zinawakabili watu (Gouldin, 1961).

Nadharia ya Uhalisia iliasisiwa na Gustave Flaubert ambaye alieleza kuwa, mtu hufikiria kwa kichwa na wala si kwa moyo wake (Gouldin, 1961). Habib (2005) anafafanua zaidi lengo la Nadharia ya Uhalisia kuwa ni kuonesha uhalisia na usahihi unaohusu ulimwengu halisi unaoonekana kwa mwanadamu. Habib anafafanua zaidi kuwa ili kufikia hatua hii, uhalisia unahitaji kuwapo kwa maelezo ya kina, kuachana na umazingaombwe, udhahania na badala yake wahusishwe wahusika kutoka katika matabaka yote badala ya kushughulika na tabaka tawala tu katika kuelezea jambo. Nao Wafula na Njogu (2007) wanaeleza kwamba, dhana ya Flaubert ilisisitiza umuhimu wa kueleza na kubainisha matatizo ya kijamii katika uhalisi na uyakinifu. Nadharia ya Uhalisia ilitumiwa kwa mara ya kwanza katika fasihi nchini Ufaransa mnamo mwaka 1850 kwa lengo la kuelezea kazi za sanaa zilizojikita katika kusawiri ulimwengu kama ulivyo (Qusby, 1988). Miongoni mwa wanafasihi wa Kifaransa waliotumia nadharia hii ni Jules Husson Champfley aliyewachora wahusika wake kulingana na mazingira halisi ya jamii (Gouldin, 1961). Kwa mujibu wa Wamitila (2002), uhalisia unasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Maelezo ya Wamitila yanaungwa mkono na Mulokozi (2017) anayeeleza kuwa wafuasi wa nadharia hii walishikilia kwamba, fasihi inapaswa kuyasawiri maisha kama yalivyo.

Nadharia ya Uhalisia iliwekewa misingi na mwanafalsafa Hegel (1979) katika kitabu chake kinachojulikana kama *Introduction to Aesthetics.* Baadhi ya misingi hiyo ni: hujikita katika mambo yaliyopo, tukio mahususi na matokeo yanayoweza kuthibitika. Kulingana na umahususi wa makala hii, uchambuzi na uwasilishaji wa data umeongozwa na misingi miwili ya Nadharia ya Uhasilia. Msingi wa kwanza ni ule unaodai kuwa uhalisia hudhihirika kupitia uhusiano kati ya mwandishi, matini na msomaji kuliko kuzingatia masuala yaliyotokea kabla. Msingi wa pili unadai kuwa mtunzi huchagua wahusika ambao ni vielelezo na mifano ya watu wanaoishi katika jamii.Sababu ya kutumia nadharia hii ni kwamba, inaangalia zaidi matukio ya kweli katika ulimwengu halisi (Mearsheimer, 2002). Kwa hiyo, nadharia hii imekuwa faafu kwani ndiyo imeuongoza utafiti huu wakati wa kuchambua kipengele cha mandhari na kueleza namna usaliti unavyosawiri uhalisia katika mandhari halisi.

## 5.0 Matokeo ya Utafiti na Mjadala

Data za utafiti zimedhihirisha kuwa, sehemu kubwa ya mandhari katika mashairi teule zimetumiwa na mtunzi ili kuujenga usaliti kwa kurejelea shughuli mbalimbali za kijamii. Mandhari zilizobainishwa ni pamoja na mandhari ya Afrika, ufukweni, sehemu za ibada, ikuluni na hospitalini. Sehemu inayofuata ni mjadala wa jinsi mandhari zinavyoujenga usaliti katika mashairi teule:

### 5.1 Tendo Linalofumbatwa Ndani ya Hisani

Utafiti huu umebaini kuwa, mandhari ya Afrika imeujenga usaliti katika diwani teule kama tendo linalofichwa ndani ya hisani. Crescent (2011) anaeleza kuwa

hisani ni tendo linaloonesha uhusiano wa karibu kati ya taifa lenye nguvu dhidi ya taifa lisilo na nguvu kiuchumi. Kulingana na utafiti huu, mtunzi wa diwani teule amelisawiri tendo la usaliti kama tendo linalofichwa ndani ya hisani kupitia ufadhili usiokuwa na tija yoyote ya kimaendeleo katika jamii za Afrika. Aidha, misaada mingi inayoingizwa Afrika na mataifa ya Ulaya haina tija kwa Waafrika kwa sababu imelenga kuwanyonya Waafrika na kuwadhoofisha kiuchumi na kijamii. Katika shairi la "Tiba Isotibu" mwandishi anasema:

1. Twajua,
   Inaumwa Afrika,
   Sana inaatilika,
   Taabani yateseka,
   Roho yake yakatika,
   Yataka tiba.
2. Bahati,
   Dakitari wa Ulaya,
   Huruma imemwingiya,
   Kaja kuisaidiya,
   Kikweli mejitoleya,
   *Kuleta tiba.*
3. Lakini,
   Vidonge chungu ajabu,
   Dawa zake hazitibu,
   Zinazidisha tabu,
   Mgonjwa kumwadhibu,
   Haipo tiba.

Dondoo hilo hapo juu linaonesha namna mandhari ya Afrika inavyoujenga usaliti kama chanzo kikubwa cha changamoto nyingi zinazosababishwa na usaliti wa nchi za Ulaya. Aidha, mandhari ya bara la Afrika imetumiwa na mwandishi kuonesha kuwa imeujenga usaliti wa nchi za Ulaya dhidi ya bara la Afrika kama tendo lililofumbatwa katika hisani. Hali hii inatokana na sababu kwamba Afrika ni bara ambalo haliwezi kujisimamia katika nyanja mbalimbali za kimaisha yakiwamo matibabu na badala yake inategemea hisani kutoka nchi za Ulaya. Mathalani, mwandishi ametumia vidonge kumaanisha misaada ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kutoka Ulaya kuashiria usaliti unaofanywa na bara la Ulaya dhidi ya Afrika. Maarifa kutoka Nadharia ya Uhalisia yanayodai kuwa mwandishi hutilia maanani mandhari katika kazi yake ya bunilizi yameuongoza utafiti huu kubaini kuwa pamoja na Afrika kufadhiliwa, ni wazi kuwa mandhari ya Afrika imetumiwa kama sehemu ya kupeleka hisani ambayo inalenga usaliti unaokusudia kuchukua malighafi kutoka Afrika. Hali hii inaonesha kuwa hisani kutoka nchi za Ulaya katika bara la Afrika si tiba, bali ni usaliti ambao umekuwa chanzo cha bara la Afrika kuendelea kuteseka kwa kutwishwa mzigo mkubwa wa madeni.

### 5.2 Tendo Linalokumbatiwa katika Kivuli cha Uongozi

Katika utafiti huu, mandhari ya Afrika imetumika kujenga usaliti kama tendo linalokumbatiwa katika kivuli cha uongozi. Usaliti unajengwa na viongozi wa Afrika kutokana na kuwapo kwa uongozi usiozingatia misingi ya kidemokrasia katika kuongoza. Kwa mujibu wa Yunus (2013), ili kuupinga usaliti, jamii inapaswa kuelewa jukumu la kuwachagua viongozi waaminifu na wenye uchungu na maendeleo ya umma. Jukumu hilo likifanyika kwa ufanisi litawaepusha kuwa na viongozi wadhulumaji. Kupitia shairi la "Madikteta" mwandishi anasema:

Katika,
Dunia hii ya tatu,
Na hasa **Afrika yetu**,
Itele "Mungu watu"
Bokasa, Idi, Mobutu,
Mizinga nayo mitutu,
Haitoi risasi,
Hutoa maraisi,
Walio madikteta.

Dondoo hili linaonesha namna mandhari ya Afrika ilivyoweza kuujenga usaliti kama tendo linalokumbatiwa katika kivuli cha uongozi. Dondoo hili linarejelea dhamira mbaya waliyonayo viongozi wengi wa Afrika dhidi ya demokrasia ya kweli. Aidha, Massoud (2018) anaeleza kwamba, viongozi wengi wa Afrika wanaendeleza masilahi binafsi kwa kupenda kujinufaisha wao wenyewe kwa badala ya kushughulikia masilahi ya taifa. Hali ya kukosa uzalendo inasababisha nchi nyingi katika bara la Afrika kukosa maendeleo (Salim, 2015). Suala hili limebainishwa kupitia uongozi wa kiimla ulioendelezwa na marais, Bokasa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Afrika ya Kati tangu 1966 hadi 1979 alipopinduliwa, Idi Amin aliyekuwa mtawala nchini Uganda tangu mwaka 1971 hadi 1979 alipoikimbia nchi, na Mobutu aliyekuwa Rais wa Zaire (zamani ikijulikana kama Kongo) kati ya mwaka 1965 hadi 1997 Laurent Kabila aliposhika madaraka na kuongoza. Hivyo, ni wazi kuwa mandhari ya Afrika inaujenga usaliti kama tendo lililokumbatiwa katika kivuli cha uongozi na ndiyo chanzo cha Afrika kutokuwa na amani. Aidha, msingi wa Nadharia ya Uhalisia unadai kuwa mwandishi hutilia maanani mandhari katika kazi yake ya bunilizi. Kulingana na msingi huu, ni wazi kwamba mandhari ya Afrika haina utulivu. Miongoni mwa masuala yanayosababisha mandhari hiyo kukosa utulivu ni uongozi wa kiimla uliokuwa umejificha katika hali ya uzalendo huku wananchi wakiishi kwa tabu ambayo chanzo chake ni usaliti wa viongozi.

### 5.3 Tendo Linalotumika Kutekeleza Azma ya Mauaji

Kupitia data iliyopatikana, imebainika kuwa mandhari ya bahari imeujenga usaliti kama tendo linalotumika kutekeleza azma ya mauaji. Kama ilivyoelezwa na Salim (2015), mauaji ni suala linalotokana na uhasama usio na mipaka kati ya mtu na mtu. Kwa mfano, shairi la "Sikuliwa Sikuzama" linaonesha ukubwa wa tatizo la

umaskini katika jamii. Kupitia shairi hilo, mhusika wa nafsi ya kwanza ametumika kubainisha namna mandhari ya bahari ilivyoujenga usaliti kama tendo linalotumika kutekeleza azma ya mauaji ya mhusika nafsi ya kwanza katika bahari. Mtunzi anasema:

**Sikuliwa Sikuzama**
Sikuliwa sikuzama,
Si hayati ni mzima,
Nimefika **ufukweni**,
Ingawa taabani,
Nimeloa chapachapa,
Na kisasi takilipa,
Bila ya huruma,
*Ni ole wao!*

Walitaka niwe chambo,
Baharini niwe shombo,
Huku natapatapa,
Ni karamu ya papa,
Wajitambe nchi kavu,
Wajigambe ni werevu,
Kamwe halikuwa,
*Izara wao!*

Katika dondoo hili, kuna mandhari ya baharini na ufukweni. Utafiti huu umebaini kuwa licha ya mandhari hizi kutumiwa kwa ajili ya shughuli za kijamii, hali ni tofauti katika utafiti huu kwani matendo ya uuaji yamekuwa yakifanyika katika mandhari hizo tofauti na matumizi yake yaliyoidhinishwa kijamii. Utafiti huu umebaini kuwa mandhari ya baharini na ufukweni zimetumiwa katika mauaji ya watu wanaosimama kinyume na utawala uliopo madarakani. Licha ya viongozi wa nchi kuaminiwa kuwaongoza wananchi, usaliti umekuwa chachu ya kuwaua au kuwapoteza watu wote wanaokuwa kinyume na matakwa ya nchi. Aidha, data hiyo inaonesha kuwa mauaji yanafanywa na watu wenye mamlaka ambao hawapo tayari kukosolewa. Licha ya kuwa viongozi wenye kujitamba kama werevu, uongozi wao unatumika kutekeleza mauaji ya watu wanaowakosoa. Aidha, sababu kubwa ya mandhari ya baharini kutumika kwa vitendo vya mauaji, imeelezwa na Zammit (2020) kuwa ni mandhari yenye mkanganyiko wa shughuli mbalimbali za kibinadamu na zile za asili kama vile kuogelea na kubarizi. Kwa hiyo, ni vigumu wakati fulani kujua kinachoendelea kutokana na mkanganyiko huo. Aidha, viongozi hutumia mandhari ya baharini na ufukweni kwa namna ya kificho, hali inayoifanya serikali kukana wakati wote kuhusika na matukio ya utekaji na mauaji.

### 5.4 Tendo la Unafiki

Mandhari ya nyumba za kuabudia imetumiwa na mwandishi katika mashairi teule kuujenga usaliti unaofanywa na viongozi wa dini za Kiislamu na Kikristo. Kama ilivyoelezwa na Malugu (2016), dini isipotumiwa ipasavyo inaweza kutazamwa kama asasi inayoweza kusababisha maangamizi, utengano, ukandamizaji, unyonyaji na unyanyasaji. Kupitia shairi la "Uasi" linaloonesha matendo machafu ya viongozi wa dini ya Kikristo na Kiislamu, mtunzi ameusawiri usaliti kupitia matendo ya viongozi wa dini ambayo yameonekana kuwa kinyume na matarajio ya dini husika. Mtunzi anasema:

**Uasi**
Katika dini,
Masheikh na Masharifu,
Mapadri na maaskofu,
Kauli zao nadhifu,
Hujigamba waongofu,
Wengi wao ni wachafu,
Wenye vitendo dhaifu
Dini wanazikashifu,
*Wanafiki.*

Katika dondoo hili, imebainika kuwa mandhari za nyumba za ibada zinatumiwa na viongozi wa dini kuficha uovu wao kwa kujigamba kuwa ni watakatifu wakati maisha yao ni machafu. Hali ya viongozi wa dini kujigamba kuwa wasafi wakati matendo yao ni machafu inaonesha wazi namna mandhari ya nyumba za ibada zinavyoujenga usaliti kama tendo la kinafiki. Aidha, licha ya waumini kuwa na imani kubwa kwa viongozi wa dini, utafiti huu umebaini kuwa viongozi wengi wa dini kama vile masheikh na masharifu, mapadri na maaskofu ni wanafiki (Ng'etich, 2011). Msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaodai kuwa uhalisia hudhihirika kupitia uhusiano kati ya mwandishi, matini na msomaji kuliko kuzingatia masuala yaliyotokea kabla, umeuongoza utafiti huu kubaini kuwa usaliti wa viongozi wa dini ndiyo chanzo cha unafiki. Hivyo, ni wazi kuwa kauli na matendo ya viongozi katika mandhari ya nyumba za ibada yanaakisi uhalisia wa maisha ya kinafiki wanayoishi baadhi ya viongozi wa dini ya Kikristo na Kiislamu katika jamii wanayoiongoza.

### 5.5 Tendo Linalotumika Kuendeleza Matabaka

Data ya utafiti huu inaonesha kwamba, mandhari ya ikuluni imeujenga usaliti kama tendo linalotumika kuendeleza matabaka katika jamii. Matabaka ni chanzo cha matatizo mengi kwani baadhi ya watu hukosa huduma za msingi kutokana na kipato duni (Shivji, 2006). Shairi la "Wasakatonge" linaonesha jinsi maskini wanavyotokwa jasho kwa lengo la kupambana na umaskini. Kadhalika, mtunzi ameonesha jinsi mandhari ya ikuluni ilivyousawiri usaliti wa viongozi wa serikali unaotumiwa katika kuendeleza tabaka kati ya viongozi wa serikali na wapiga kura wao. Mwandishi anasema:

**Wasakatonge**
Wao huweka serikalini,
Wanasiasa madarakani,
Dola ikawa mikononi,
Wachaguliwa wa **ikuluni,**
Lakini wachaguaji duni.

Kwa kuchunguza dondoo hili, ni dhahiri kwamba kupitia mandhari ya ikulu usaliti umejengwa kama tendo linaloendeleza matabaka kati ya viongozi waliochaguliwa na wananchi dhidi ya wapiga kura kwa ajili ya masilahi binafsi. Kupitia mandhari hii, mtunzi ameonesha kuwa wanasiasa wakishaiweka dola mikononi mwao, huendeleza matendo ambayo ni kinyume na ahadi wanazozitoa wakati wa kuomba kupewa nyadhifa hizo. Suala hili linathibitisha uhalisia uliopo katika jamii hususani wanasiasa wanaoingia madarakani wakitanguliza masilahi yao binafsi huku wapiga kura wao wakiishi maisha duni. Kutokana na ufafanuzi huo, makala hii inakubaliana na Yunus (2013) anayedai kuwa siasa ya nchi ndiyo iamuayo hatima ya nyanja nyingine za maisha. Kwa mantiki hiyo, usaliti na siasa ni masuala yanayooana na hutumiwa kwa masilahi binafsi ya viongozi waliopo madarakani.

## 5.6 Tendo Linalotumiwa Kuonesha Sababu za Huduma Mbovu za Kiafya

Katika uchambuzi wa mashairi teule, imebainika kuwa mandhari ya hospitalini imeujenga usaliti kama tendo linaloonesha sababu za huduma mbovu za kiafya hospitalini. Mohochi (2011) anadai kuwa wasomi, hasa waliopewa dhamana ya kuhudumia afya za watu, wana nafasi kubwa ya kuhakikisha jamii zipo salama kiafya. Suala hili linamaanisha kwamba, kupitia mandhari ya hospitalini watoa huduma za afya hutekeleza azma yao ya usaliti dhidi ya wananchi kwa kutoa huduma kinyume na misingi ya kanuni za kiafya. Suala hili limeoneshwa na mtunzi katika diwani ya *Wasakatonge* kupitia shairi la “Mumiani” linaloonesha jinsi wahudumu wa afya wanavyotoa huduma za afya bila kuzingatia ubora na maadili ya kitabibu. Mtunzi anasema:

**Mumiani**
1. Mumiani,
Mijini,
Watembea kwa matao,
Kuzifanya kazi zao,
Kuzinyonya damu zetu,
Hawangoji,
*Tulale.*

2. Mumiani,
Hospitalini,
Wagonjwa hupasuliwa,
Sindano hushindiliwa,

Kuzitoa damu zetu,
Hawasubiri,
*Tulale.*

Dondoo hilo linaonesha kuwa, usaliti umejengwa kupitia mandhari ya hospitalini ambayo si salama kutokana na kuvamiwa na mumiani. Taswira ya mumiani imetumiwa katika beti namba moja na mbili za shairi la "Mumiani" kuwakilisha viongozi na wafanyakazi wanaohudumia wagonjwa bila kuzingatia huduma bora za kiafya. Kupitia mandhari ya hospitalini, viongozi wa Afrika ni wasaliti kutokana na kazi zinazofanywa bila kuzingatia ubora wa tiba. Kazi hizo ni kupasuliwa kwa wagonjwa na kuchomwa sindano. Vitendo hivi vinavyofanywa na mumiani vinadhihirisha wazi hali ya usaliti unaofanywa na viongozi na wahudumu walioaminiwa kuhudumia afya za watu katika jamii.

Suala la usaliti hospitalini linaelezwa pia na Brennan (2006) kwamba unyonyaji unafanywa na viongozi au watu wa tabaka la juu dhidi ya tabaka la chini. Unyonyaji unaofanywa katika mandhari za hospitalini huwaathiri wananchi wanaoishi mijini na vijijini. Kwa maana hiyo, wagonjwa hutawaliwa na hofu na vitisho kutokana na kupasuliwa na kuchomwa sindano, hali inayohatarisha uhai wao. Aidha, msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaodai kuwa mandhari humsaidia mtunzi kuwasuka wahusika wake unadhihirisha hali halisi ya usaliti wa viongozi na wahudumu wa hospitalini wanavyojenga hofu kwa wagonjwa badala ya kuwapatia huduma bora za kiafya.

## 5.7 Tendo Linalotumiwa Kuonesha Athari za Kufadhiliwa

Utafiti huu umebaini kuwa, mandhari ya mabaraza bungeni imeujenga usaliti kama tendo linalotumika kuonesha athari za nchi za Afrika kufadhiliwa. Aidha, katika kazi teule imebainika kuwa miongoni mwa madhara ya taifa kufadhiliwa ni kupitishwa kwa sera za wafadhili na kisha kuamuliwa na wafadhili kuzitekeleza bila kujali masilahi mapana ya nchi. Kwa mfano, katika diwani ya *Wasakatonge* utafiti huu umebaini kuwa, ufadhili wa mataifa ya Ulaya ni chanzo cha usaliti unaosababisha kutungwa kwa sera na sheria zinazopitishwa bungeni na wabunge kwa lengo la kuwanufaisha wafadhili kuliko taifa. Hali hii inawaacha watu wa hali ya chini wakiishi maisha ya taabu. Suala hili limethibitishwa katika shairi la "Wafadhiliwa" linalosema:

**Wafadhiliwa**

1. Wafadhili kufurahishwa,
Ni sera zao kupitishwa,
Rais anaamrishwa,
*Tekeleza*!
2. Mawaziri wanajulishwa,
Sheria zinabadilishwa,
Na bungeni kuhalalishwa,

*Pitisheni*!
3. Ni sera za kunakamishwa,
Umma wote kuatilishwa,
Shida na dhiki kuvalishwa
*Taabani!*
4. Taifa linadhalilishwa,
Mambo mengi kushurutishwa,
Na bila kushirikishwa,
*Yaoneni*!

Katika dondoo hilo, imebainika kuwa taifa linapofadhiliwa hulazimika kutekeleza matakwa ya wafadhili kuliko ya taifa lenyewe. Mathalani, utafiti huu umebaini kuwa katika ubeti wa kwanza mtunzi anaonesha madhara ya usaliti kwa taifa yanayotokana na kufadhiliwa. Miongoni mwa madhara hayo ni kupitishwa kwa sera za wafadhili ambapo rais anaamrishwa kutekeleza licha ya kutokuwa na manufaa kwa taifa lake. Kwa hiyo, usaliti husababisha taifa kulazimika kutekeleza sera za nje zisizo na manufaa kwa watu wa tabaka la chini. Kadhalika, imebainika kuwa usaliti dhidi ya taifa hufanywa na wapitisha sheria na sera hizo za Ulaya unaofanywa na wabunge na mawaziri waliopewa dhamana na wananchi kuwakilisha matatizo yao bungeni. Hata hivyo, Ramadhani (2005) ameonesha kuwa, kufadhili ni kusaidia kwa hali na mali ili taifa liweze kufikia matarajio yake. Hoja hii inaungwa mkono na Guillem (2012) kuwa, ufadhili ni suala la upendo na hiari, na haliwezi kulazimishwa. Kwa upande wa utafiti huu, suala la ufadhili limebainika kuwa chanzo cha mateso katika nchi zinazoendelea hususani Afrika kutokana na usaliti unaofanywa na viongozi wa mataifa yaliyoendelea. Vilevile, msingi wa Nadharia ya Uhalisia unaodai kuwa mtunzi huchagua wahusika ambao ni vielelezo na mifano ya watu wanaoishi katika jamii, umeuongoza utafiti huu kubaini mandhari ya bungeni. Mandhari hii ya bungeni imetumiwa kuonesha namna usaliti unavyotumiwa na wabunge na mawaziri kuliingiza taifa kwenye matatizo kutokana na kupitisha sera zisizo na tija kwa taifa.

## 6.0 Hitimisho

Makala hii imechambua mandhari katika ujenzi wa usaliti katika diwani ya *Wasakatonge*. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba mwandishi wa diwani teule ameiumba mandhari katika mashairi teule kwa kuyanasibisha kwa karibu na suala la usaliti katika uongozi, elimu, siasa, dini na jamii kwa ujumla. Kadhalika, mandhari kama vile Afrika, bungeni, ikuluni, hospitalini, nyumba za kuabudia, ufukweni na baharini ni mandhari halisi zilizousawiri usaliti katika mtazamo hasi usio na manufaa kijamii, kisiasa, kidini na kiafya. Makala hii imechangia maarifa kuhusu mandhari na usaliti katika fasihi kupitia ushairi wa Kiswahili kiasi cha kupanua uelewa wa namna kipengele cha mandhari kinavyoujenga usaliti katika ushairi kama ilivyo katika tanzu nyingine za riwaya, tamthiliya na hadithi fupi.

**Marejeleo**

Brennan, J.R. (2006) "Blood Enemies: Exploitation and Urban Citizenship in The Nationalist Political Thought of Tanzania". *Journal of African History*. Juz. Na. 47: 389-413. Inapatikana katika https://core.ac.uk. Ilisomwa tarehe 23 Februari 2023.

Crescent, L. (2011) *A Definition of Charity*. ACT 2600: Commonwealth of Australia.

Dargan, E. P. (2013) *Studies in Balzac's Realism*. Chicago: Literary Licensing, LLC.

Goodwyn, F. (1978) New Light on the Historical Setting of Garcilaso's Poetry. *Hispanic Review*, Juz. Na. 46(1): 1-22. Inapatikana katika https://www.semanticscholar.org. Imesomwa tarehe 10 Agosti 2024.

Gouldin, G. (1961) *Realism.* Richmond: University of Richmond.

Habib, M.A.R. (2005) *Modern Literary Criticism and Theory: A History.* USA: Blackwell Publishing.

Hegel, G.W.F. (1971) *The Spirit of Christianity and Its Fate in Early Theological Writings*(T. M. Knox, Mfasiri) Chicago: Chicago University Press.

Khatib, M.S. (2003) *Wasakatonge*. Nairobi: Oxford University Press (T) Limited.

Kuntz, M. (1993) *Narrative Setting and Dramatic Poetry*. New York: Brill.

Malugu, A. (2016) "Nafasi ya Fasihi katika Kusawiri Suala la Dini". *Kiswahili*, Juz. Na. 79: 66-77.

Mohochi, E.S. (2011) "Mielekeo ya Wasomi wa Kiswahili na Viongozi wa Afrika Mashariki kuhusu Lugha ya Kiswahili." *Swahili Forum*, Juz. Na. 18: 24-36.

Mulokozi, M.M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Oing, T. (2017) *The Effect of Betrayal on Task Co-Representation*. Shahada ya Umahiri katika Saikolojia (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha New Jersey.

Rachman, S. (2010) "Betrayal A Psychological Analysis." *Behaviour Research and Therapy*, Juz. Na. 48: 304-311. Inapatikana katika https://pubmed.ncbi.nlm.nih.gov. Ilisomwa tarehe 20 Agosti 2024.

Wafula, R.M. na Njogu, K. (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wisemasn, J.P. na Duck, S. (1995) "Having and Managing Enemies: A Very Challenging Relationship". *Comfroting Relationship Challenges*, Juz. Na. 85: 43-72. Inapatikana katika https://www.semanticscholar.org. Ilisomwa tarehe 30 Juni 2024.

Zammit, M.L. (2020) *A Critical Analysis of Beach Management Systems and Processes on the Maltese Islands, Focusing on Public and Key Stakeholder Perceptions*. Tasnifu ya Uzamivy (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Portsmouth, London.